

Miunganiko baina ya wakimbizi na wenyeji kwa ufumbuzi wa ndani: Mafunzo kutoka Tanzania

Tanzania ina wakimbizi wapatao 264,475 waliosajiliwa; karibia asilimia 85 ya wakimbizi hawa wanaishi katika kambi (UNHCR, 2021) wakati idadi nyingine ya wakimbizi wanaishi nje ya kambi ya wakimbizi, mara nyingi katika maeneo ya mijini. Katika jiji la Dar es Salaam, ambalo lina idadi ya watu wapatao milioni 6.7, idadi rasmi ya wakimbizi wanaoishi katika jiji hilo haifiki 300, wakati makadirio yanaonyesha kwamba kuna wahamiaji wapatao elfu kumi wanaoishi katika mazingira magumu na wenye hali kama ya wakimbizi.

Sheria ya wakimbizi ya Tanzania ya mwaka (1998) imefanya kuwa ni kosa kuishi nje ya kambi ya wakimbizi bila kibali cha serikali. Hata hivyo uhamaji kutoka kambini kwenda Dar es Salaam sio jambo lisilo la kawaida, na wala haliko katika mwelekeo mmoja tu. Ni wakimbizi wachache tu wanaotaka kuondoka kambini na kujenga maisha Dar es Salaam amba wanafanikiwa kupata kibali cha kufanya hivyo. Wengi wao wanalazimika kuita ‘njia zisizo rasmi’ na kuijunga na wahamiaji wengine walio katika mazingira magumu na kama ya wakimbizi wanaoishi kwa siri mijini. Pasipokuwa na muinganiko na mahusiano baina ya wakimbizi na wenyeji, wakimbizi hawa wa mijini wanalazimika kuficha utambulisho wao na kupelekea hatari ya kuishi daima katika hali ya kutengwa, kuhamahama na kutokuwa sehemu ya jamii waliyomo.

“Wasamaria wema” kama viunganishi

Wakihamashwa na maadili ya kidini na ya kiutu, baadhi ya Watanzania huwasaidia wahamiaji wenye uhitaji. Hawa “wasamaria wema” mara kwa mara wamewasaidia wakimbizi kupata makazi, chakula, au pesa za usafiri. Baadhi hutoa misaada hii kwa sababu ya uwezekano wa kushirikiana katika siku za baadaye. Kwa mfano shirika la DIGNITY Kwanza limejifunza kwamba Watanzania amba wameishi na wakimbizi wanaamini kwamba wanaweza kujifunza utaalamu wa wakimbizi na kushirikiana nao katika biashara. Kwa kushirikiana na wakimbizi, Watanzania wanapata fursa wa kutumia mitandao na rasilimali za wakimbizi. Katika biashara ya vitenge, kwa mfano, ununuzi na usafirishwaji wa vitenge kutoka Kongo unawezekana kupitia mahusino na Wakongo. ‘Wasamaria

“Mwingiliano na wakimbizi wa mijini amba hawana vibali vya ukaazi umeonyesha kwamba wanatamani kupata vibali hivyo.”

wema’ wamekuwa na mchango muhimu sana katika kuwawezesha wakimbizi wa mijini kupata huduma za umma na kuwafanya kuwa sehemu ya jamii.

Zaidi ya mahusiano hayo ya kibinagsi, mashirika ya kitanzania, jitihada za wahamiaji wenyewe, na mashirika ya kidini huwasaidia wakimbizi. Kati ya mwaka 2018 na 2019, ‘DIGNITY Kwanza’, kwa mfano, ilitekeleza mradi wa “biashara ya pamoja” mradi ulio chini ya programu yake ya uwezeshaji wa jamii. Mradi unajumuisha mafunzo ya ujuzi wa biashara kwa wakimbizi na wanajamii wenyeji. Baada ya mafunzo, washiriki walitakiwa kuunda makundi ya watu wawili wawili: mkimbizi mmoja na Mtanzania mmoja. Kila kundi lilitakiwa kutengeneza mpango wa biashara ya pamoja. Kati ya makundi 25, makundi nane yaliyofanya vizuri zaidi yalipatiwa zawadi ya shilingi za kitanzania milioni mbili kwa kila kundi (Sawa na

EUR 800) kwa ajili ya kuwasaidia kuwekeza katika biashara yao. Biashara zilizozawadiwa ni pamoja na migahawa midogo iliyopo kando ya barabara, duka la ushonaji, saluni ya kike, biashara ya mitumba na biashara ya nafaka. Wakati ni watanzania pekee wanaoweza kusajili biashara kisheria, mkimbizi anaweza kuweka ujuzi wake katika vitendo. Mradi huu wa “biashara ya pamoja” ni ushahidi wa jinsi ushirikiano kati ya watanzania na wakimbizi unavyoleta matokeo ya manufaa kwa pande zote mbili; na unawawezesha wajasili mali wakimbizi na raia wa Tanzania, kuanzisha shughuli za kuwapatia riziki katika jiji la Dar es Salaam.

Hadhi ya kisheria na miunganiko baina ya wakimbiza na wenyeji


Hadhi ya kisheria, au ukosekanaji wake vina athari ya moja kwa moja katika suala la uhamaji na miunganiko baina ya wakimbizi na wenyeji. Uwezo wa kuungana na kuhama kwa uhuru, kuwa na uwezo wa kupata huduma za umma (elimu, afya) na msaada katika mashirika, kwa kiasi kikubwa vinategemea kama, mkimbizi wa mijini amesajiliwa ama la; mkimbizi aliyesajiliwa anaonekana kwamba anakuwa na hali nzuri kuliko yule ambaye hajasajiliwa.

Wakimbizi wa mjini ambao hawajasajiliwa wanalazimika kusaidiwa na wenyeji kupokea misaada kutoka kwa rafiki au ndugu zao walio nje ya nchi, kusajili biashara zao, kupata huduma za umma na mara nyingi huwa sio wanufaika au walengwa wa programu nyingi za mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO). Kwa mfano, wakimbizi pekee wa mjini ambao walikuwa na nyaraka za kiserikali zinazoonyesha uhalali wao wa kukaa nchini ndio waliweza kushiriki katika mradi wa “biashara ya pamoja” uliotekelizwa na DIGNITY Kwanza. Vile vile wakimbizi wengi wa mjini ambao hawajasajiliwa walipoteza mawasiliano ilipokuja sheria ya kusajili laini za simu kwa kutumia kitambulisho cha taifa mnamo Januari 2020 (wakimbizi waliosajiliwa wanaweza kutuma maombi ili kupata kitambulisho cha Taifa). Kwa wengi simu hazikuwa tu chombo cha mawasiliano, pia walizitumia kama ‘ofisi zao’ sehemu ambayo wangeweza kutangaza bidhaa na huduma zao, kukutana na wateja wao muhimu na kupokelea malipo.

Mwingiliano na wakimbizi wa mjini ambao hawana vibali vya ukaazi umeonyesha kwamba wanatamani kupata vibali hivyo. Baadhi waliomba vibali vya wakulima (peasant permit) vilivyotolewa na Idara ya Uhamiaji kati ya 2011 na 2012. Pia waliitikia wito wa Idara ya Uhamiaji kwenda kujisajili, hata bila

kujuua lengo kamili la usajili huo, wakitumaini kwamba unaweza kupelekea kupata namna fulani ya utambulisho wa kisheria. Hali ya wakimbizi wa mijini kutokuwa na hati za kuishi nchini na mijini kwa kiasi kikubwa inatokana na kutokuwepo njia ambazo wanaweza kuzimudu kifedha au kimasharti mengine.

Watendaji wa serikali na wasio wa kiserikali wanaweza kuhamasishwa na wenyeji katika kujenga uhusiano na wakimbizi. Nchini Tanzania wakimbizi wengi wanajua ni nini wanahitaji na ni mchango gani wanaweza kuwa nao kuliko wajauavyo watendaji wa serikali na wasio wa serikali. Kama suala la utendaji mzuri, wakati wote watendaji wanatakiwa kuwahusisha watu ambao wamewalenga kuwatumikia kabla hawajatoa maamuzi ambayo yanawaathiri watu hao. Katika baadhi ya kesi, wenyeji, wakimbizi, mashirika na makanisa yameshachukua hatua ili kuboresha hali zao. Hatua zinatakiwa kuchuliwa ili kuwapatia wakimbizi wa mijini hadhi ya kisheria na kuwezesha uhamaji wa kisheria kutoka katika makambi na kwenda maeneo ya mijini. Hili sio tu kwamba litawapa wakimbizi waliopo mjini uhuru wa kiuchumi, lakini pia litawanufaisha raia wa Kitanzania wanaoshirikiana nao; ili mwishowe wote waweze kuishi maisha ya heshima.



© Caitlin Katsiaficas (ICMPD)

Dokezo hili linatokana na kazi ya [Wilson, C. et al. \(2021\). Figurations of Displacement in and beyond Tanzania: Reflections on protracted displacement and translocal connections of Congolese and Burundian refugees in Dar es Salaam \(TRAFIG working paper no. 8\). Bonn: BICC.](#)
DOI: [10.5281/zenodo.5841878](https://doi.org/10.5281/zenodo.5841878)

The contents of the document are the sole responsibility of the authors and do not necessarily reflect the views of the European Union. The European Commission is not responsible for any use that may be made of the information it contains.



This project has received funding from the European Union's Horizon 2020 research and innovation programme under grant No 822453

Contact

Dr Benjamin Etzold

BICC

Pfarrer-Byns-Str. 1, 53121 Bonn • phone +49 (0)228 911 96-24
contact@trafig.eu • www.trafig.eu • Twitter @TRAFIG_EU

Authors: Janemary Ruhundwa (DIGNITY Kwanza), Bishara Msallam (DIGNITY Kwanza), Catherina Wilson (ULEI), Elvan Isikozlu (BICC)

Translation: Joshua Mshani

Publication date: November 2021

DOI: [10.5281/zenodo.5898194](https://doi.org/10.5281/zenodo.5898194)



Except where otherwise noted, this work is licensed under:
creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/3.0/

Copyediting / Layout: Gizem Guelant

Editorial design: kippconcept gmbh